JINA…… NAMBA YAKO……

102/2
KISWAHILI
Karatsi ya 2
LUGHA
JULAI/AGOSTI 2010
SAA: 2 ½

MTIHANI WA MAKADIRIO
KIDATO CHA NNE 2010

MAAGIZO:

1. Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. Jibu maswali yote.
3. Andika majibu yako katika kijitabu hiki cha maswali.

Swali	Upeo	Alama
	Jumla	

1. **Ufahamu**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo.

Waajiri wengi wanazilaumu taasisi za elimu kwa kukosa kutoa wafanya kazi wenye ujuzi tosha, hasa wa teknolojia za kisasa kama kutumia kompyuta kutenda kazi mbalimbali. Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha sana.

Ujuzi wa kutumia kompyuta unaweza kumfaa mwanafunzi hata anapokosa nafasi ya kujiunga na chuo kikuu kwa vile anaweza kuendelea na elimu yake kupitia kwa elimu mtandao. Pia anaweza kufanya utafiti wa kina kupitia intaneti na kwa njia hii akaimarisha elimu yake.

Mojawapo ya njia za kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia ni kuanzishwa kwa mikakati mipya ya kufunza. Somo la kompyuta laweza kuimarika mashuleni endapo kwanza walimu watahamasishwa juu ya faida za ujuzi huu.

Kwa kutumia kompyuta kufunza, walimu wanaweza kufunza madarasa kadhaa katika kipindi kimoja bila kulazimika kuyahudhuria. Hii itapunguza kiwango cha kazi kwa walimu kwa vile watapata muda wa kufanya utafiti mpana. Aidha, watapata habari na ufahamu zaidi wa mambo kwa kutumia mitambo ya kompyuta kutoka kwenye intaneti, kupitia tovuti.

Hata hivyo mipango hii inakabiliwa na changamoto kama vile bei za juu za mitambo na vifaa vya kompyuta, ukosefu wa miundo msingi itauwezesha utumiaji wa mitambo hii na ukosefu wa walimu waliohitimu somo la kompyuta.

Pia, kuna tatizo la ukosefu wa nguvu za umeme hasa katika maeneo ya mashambani. Vile vile, katika maeneo yaya haya, wanafunzi na wazazi wengi huchukulia somo la kompyuta kuwa gumu na linalofaa wakaazi na wanafunzi kutoka maeneo ya mijini wala si muhimu kwao mashambani.

Maswali:

a). Ipe taarifa uliyosoma anwani inayoifaa. (alama 1)

……

……

b) Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha: Ni hali gani inayozungumziwa katika aya ya 1?(alama 2)

……...

……...

……

c) Ujuzi wa kutumia kompyuta unaweza kumfaidi vipi mwanafunzi? (alama 3)

……

……

……

……

d) Mikakati mipya ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia inakabiliwa na pingamizi zipi? (alama 5)

…….

…….

…….

…….

……

……

……

…….

e) Taja manufaa mawili ambayo mwalimu anaweza kupata kutokana na ujuzi wa teknolojia ya kompyuta. (alama 2)

……

……

……

f) Andika msamiati mwafaka zaidi kwa maneno yafuatayo: (alama 2)

i) Kompyuta - ……..

ii) Intaneti - ……

2. MUHTASARI/UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali

Nchi nyingi duniani zimetia saini mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Haki ni mambo mema ambayo watoto wanastahili kutendewa. Kwa kutia saini, nchi hizi zimetangaza kjitolea kwao kuzilinda na kuhakikisha kuwa hakuna ukiukaji wake na kuwa watoto wote katika himaya zao wananufaika kutokana na haki hizi.

Miongoni mwa haki hizi ni kuwa kila mtoto ana haki ya kuishi na kupata chakula cha kutosha na chenye vimilishe bora. Pili, kila mtoto ana haki ya elimu. Elimu hii inafaa kutolewa bila ada na iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Kisha, kila mtoto ana haki ya kutopigwa, kutodunishwa, kufanya kazi za kitumwa, nzito na za kushurutishwa. Hali kadhalika ana haki kuishi katika nyumba au makazi bora na salama, kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Anatakiwa ashirikishwe katika kufanya maamuzi. Fauku ya haya, ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalumu, michezo, upendo na habari. Isitoshe anastahili kuheshimiwa kimawazo na kihisia. Haki hizi zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, hiyvo serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba za nchi zao na sheria zao.

Walakini, haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. Lakusikitisha na kukera ni kuwa wanaotarajiwa kuwa vigogo vya kuzilinda haki hizi ndio wanaongoza kuzikiuka. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kunyimwa chakula, kufanyishwa kazi kipunda, kuteswa, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Kuna watoto wengi wanaolala nje. Wengine hawapati chakula, licha ya kuwa wanatakiwa kupata chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi kwani hata awamu moja ni adimu kupata.

Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Viongozi katika mataifa haya hawafanyi kitu ila kutazama tu wakati watoto wanaotakiwa kuwalinda wamegeuka mibaba ya kuua na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia huvalishwa mabuti ya kijeshi ambayo ni mizigo mizito ya kubeba mbali na bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani wakati wanatakiwa kuwa wamelindwa majumbani na shuleni na wazazi wao na serikali.

Jukwaa la vijiji vya mataifa ya ulimwengu wa tatu limesheheni watoto wasioenda shule kwa sababu ya lindi la ufukara uliokithiri. Elimu ya bure inayogusiwa katika haki za watoto haipo. Wanaong'ang'ana iwepo ni kama kwamba ni waota ndoto mchana. Jiulize, watoto wangapi sasa hivi wamo majumbani bila kwenda shuleni kutokana na ukosefu wa karo? Wangapi wamo mitaani wakivuta na kunusa gundi huku wakiombaomba vishilingi?

Hivi ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima na kuungana mikono kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu haki za watoto. Twapasa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi kushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu hukusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati bali si kwa chati.

Maswali:

a) Fupisha aya mbili za kwanza(Maneno 65-70) (alama 8)

Matayarisho

……
……
……
……
……
……
……
……

……
……

Jibu

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

b) Eleza ni vipi ukiukaji wa haki za watoto unaweza kuepukwa. (Maneno 30-35) (alama 4)

Matayarisho

……
……
……
……
……
……
……

Jibu

……
……
……

……

……

……

……

(kumbuka alama za mtiririko ni 3)

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Ainisha sentensi ifuatayo. (alama 3)

Aliyefiwa

……

……

……..

b) Sauti zifuatazo ni za aina gani? (alama 2)

(i) /w/ -

(ii) /r/ -

c) Kanusha (alama 1)

Akikimbia mbio, atashinda.

……

……

d) Andika kinyume (alama 2)

Tulipita njia nyembamba kisha tukapanda haraka na kufika kwa babu.

……

……

……

e) Unda vivumishi kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama 2)

(i) Dhulumu –

(ii) Kanusha

f) Eleza matumizi matatu ya kistari kifupi na kila mojawapo toa mfano. (alama 3)

……

……

…….

g) Tumia neno <u>oza</u> katika sentensi ili kudhihirisha maana mbili tofauti. (alama 2)

……

……

……

……

h) Changanua sentesi ifuatayo ukitumia njia ya mistari/mishale. (alama 4)

Juma alikuwa akielekea nyumbani

……

……

……

…….

…….

i)Andika kwa udogo. (alama 2)

Mwana amepatiwa pete na mbuzi

……

……

……

……

j) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 3)

Kassim: Niletee kikombe tafadhali

……

……

Emma: Mimi si mtumwa

……

……

k) Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 2)

Anapenda kusoma kuliko Makokha.

……

……

l) Eleza matumizi ya kwa katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Wazee kwa vijana walivuka barabara kwa haraka na sita kwa kumi wakafika kwa John.

……

……

……

……

m) Huku ukitoa mifano taja aina za vishazi. (alama 2)

……

……

……

……

n) Tofautisha matumizi ya 'vizuri' katika sentensi hii. (alama 2)

i) Alinunua viatu vizuri na akafungiwa vizuri.

……

……

……

……

o) Andika kwa wingi (alama 2)

i) Ukimwona mwambie aje anisalimie

……

……

……...

p) Andika maneno yafuatayo katika kauli zilizoonjeshwa katika mabano. (alama 2)

Neno	Kauli	Jibu
1. kunja	(kutendeka)	
2. safiri	(kutendesheka)	

q) Sahihisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Angalifua samaki mapema angebebwa na gari.

……

……

……

r) Fafanua maana ya misemo ifuatayo. (alama 2)

i) Hahulu kuja - …….

ii) Piga mlaza mlaza - ……

ISIMU JAMII

4. Wanaisimu jamii huchunguza misimu kama kipengele muhimu katika mazungumzo ya kila siku miongoni mwa watu mbalimbali katika jamii.

a) (i) Eleza maana ya misimu (alama 1)

……

……

(ii) Kwa kutolea mifano mwafaka, taja sifa mbili za misimu. (alama 2)

b) Eleza maana ya

(i) lugha sanifu (alama 1)

……

…….

(ii) lugha ya taifa (alama 1)

……

……

c) Fafanua pingamizi zozote tano zinazokumba ukuaji na ueneaji wa lugha ya kiswahili nchini Kenya. (alama 5)

……

……

……

……

……